




AINA 9 ZA CONTENT ZINAZOKUZA BIASHARA YAKO

Nini cha ku-post, kwa nini kinafanya kazi, na mifano unayoweza kuanza nayo wiki hii.



FREE GUIDE NA

Med · @he.is.med

IMELETWA NA

Ocular Films

KWA AJILI YA

Biashara ndogo na za kati

Kanuni moja kuu



Watu hununua kwa biashara wanayojua, wanayoipenda na wanayoiamini. Kila post ijenge moja kati ya haya matatu.

01

Wakujue

Wakuone mara kwa mara mpaka walikumbuke jina la biashara yako.

02

Wakupende


Wa-enjoy content yako na vibe ya brand yako.

03

Wakuamini

Waone proof kwamba unatimiza unachoahidi.

Content yako ina kazi tatu




Kila post ifanye kazi moja. Wageni wanakuwa followers, followers wanakuamini, na wanaokuamini wanakuwa wateja.

<p>VUTIA</p> <p>Wageni wanakugundua</p> <p>Elimisha</p> <p>Trends kwa ubunifu</p> <p>Behind the scenes</p>	<p>JENGA IMANI</p> <p>Followers wanaanza kukuamini</p> <p>Reviews za wateja</p> <p>Stori yako</p> <p>Before & after</p>	<p>UZA</p> <p>Wanaokuamini wanakuwa wateja</p> <p>Onyesha bidhaa</p> <p>Jibu maswali</p> <p>Ofa za kweli</p>
--	---	--

Biashara nyingi zina-post matangazo ya 'nunua' tu. Ndiyo maana post zao za mauzo haziuzi.

Kazi ya 1: Vutia watu wapya



Content ambayo watu wanai-enjoy, wanai-save na kui-share, hata kabla hawajakujua.

Elimisha

Tips fupi na kuondoa dhana potofu. Ukifundisha, unaonekana mtaalamu.

JARIBU HII

"Makosa 3 watu hufanya wakinunua ____."

Trends kwa ubunifu

Tumia sound au meme maarufu, ila iwe kuhusu biashara yako.

JARIBU HII

Trending sound juu ya siku yako yenye kazi nyingi zaidi.

Behind the scenes

Onyesha jinsi mzigo unavyotengenezwa, kupakiwa au kufikishwa. Uhalisia unashinda ukamilifu.

JARIBU HII

"Tunapack oda za leo" ndani ya sekunde 15.

Kazi ya 2: Jenga imani



Proof kwamba wewe ni halisi, unaaminika na unastahili hela yao.

Reviews za wateja

Mteja halisi akiongea kwa maneno yake anaaminika kuliko chochote utakachosema wewe.

JARIBU HII

Video fupi ya mteja aliyeridhika au screenshot ya WhatsApp (kwa ruhusa yake).

Stori yako

Watu hu-follow watu. Sura yako na safari yako vinaipa brand utu.

JARIBU HII

"Kwa nini nilianzisha biashara hii" ndani ya sekunde 30.

Before & after

Onyesha mabadiliko unayoleta. Matokeo yanaongea kuliko maneno.

JARIBU HII

Muonekano wa zamani pembeni ya mpya baada ya huduma yako.

Kazi ya 3: Fanya mauzo

Sasa wanakuamini. Fanya kununua kuwe wazi na rahisi.



Onyesha bidhaa

Close-ups, bidhaa ikitumika, na bei kila mara.

JARIBU HII

"Bidhaa zetu 3 zinazotoka sana wiki hii."

Jibu maswali

Kila swali kwenye DM ni post inayosubiri kutengenezwa.

JARIBU HII

"Naagizaje, nalipaje na napokeaje?"


Ofa za kweli

Sababu halisi ya kununua sasa. Usitengeneze haraka ya uongo.

JARIBU HII

"Wiki hii tu: delivery bure Dar."


Hooks: wafanye watu waache kuscroll ndani ya sekunde 3



Sentensi ya kwanza ndio inaamua kama watu wataendelea kuangalia. Itamke, iandike kwenye screen, jaza nafasi.

1	"Usinunue ___ kabla hujaona video hii."
2	"Makosa 3 ambayo kila mtu hufanya na ___."
3	"Hivi ndivyo tunavyotengeneza ___, step by step."
4	"Alikuja kwetu akiwa na ___. Mcheiki sasa."
5	"Ukweli kuhusu ___ za bei rahisi."
6	"Mtumie mtu anayehitaji ___."

Mambo ya kufanya, na mambo ya kuepuka



Fanya	Epuka
Post kwa uendelevu, hata kama ni simple	Ku-post matangazo ya 'nunua sasa' tu
Onyesha watu halisi na sehemu halisi	Ku-repost video za page nyingine
Weka bei na jinsi ya kuagiza	Intro ndefu za kimya na logo kubwa
Jibu comments na DM haraka	Reviews feki au matokeo yaliyoeditiwa
Ongea lugha ya wateja wako	Kupotea kwa wiki kadhaa

Mfahamu creator



Med

[@he.is.med](#)

Filmmaker, content creator & strategist
Certified Public Accountant (CPA) · AI Native

Now nimefanikisha ukuaji wa brands mbalimbali kupitia content, zikiwemo brands zangu mwenyewe. Kila kilichopo kwenye hii pdf ni vitu ninavyovifanyia kazi kila siku kwa wateja wangu na kwenye biashara zangu binafsi.

Hii guide ya bure ni favor yangu kwako. Sasa nitafurahi kama na wewe utanifanyia favor kwa ku-follow business pages zangu.

<p>Ocular Films</p> <p>Creative production company: commercials, UGC na social media content kwa biashara.</p> <p>@ocular.films ocularfilms.com</p>	<p>TimePoint Dar</p> <p>Saa original kwa bei unayoiweza, tunakuletea popote Dar es Salaam.</p> <p>@timepointdar timepointdar.com</p>	<p>Lux Wedding Experience</p> <p>Wedding films na picha zinazokufanya uikumbuke siku yako tena na tena.</p> <p>@luxweddingexperience luxweddingexperience.com</p>
---	--	---

Unahitaji content ya biashara yako? DM [@ocular.films](#) au tembelea [ocularfilms.com](#)